

MKATABA WA KUPANGISHA

KATI YA

M/S THAKER SINGH

NA

JOSEPH BERNADO SIMKOKO

Umeandaliwa na:

Goldmark Attorneys,
Advocates,
Plot No. 13 Block "L",
Mbeya Avenue, Uhindini,
P.O.Box 1605,
DODOMA.

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu wa upangishaji umefanywa leo hii tarehe 01 Mwezi wa 02 Mwaka 2023

KATI YA

M/S THAKER SINGH wa S.L.P 62, Dodoma, ambaye katika mkataba huu atatambulika kama "**MWENYE NYUMBA**" kwa upande mmoja.

NA

JOSEPH BERNARDO SIMKUKO wa S.L.P 4169, Dodoma, ambaye katika mkataba huu atatambulika kama "**MPANGAJI**" kwa upande wa pili.

KWA KUWA mmiliki wa nyumba/chumba iliyopo/kilichopo katika katika Kiwanja Na 3-4 Kitalu 57 eneo la AREA D, KEMI STREET katika Jiji la Dodoma.

NA KWA KUWA mpangaji amehiyari kupanga eneo hilo kwa masharti yafuatayo hapa chini:

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

1. Kwamba, mkataba huu wa upangaji utakuwa wa kipindi cha Miaka/Mwaka 1 kuanzia tarehe 1/3/2023 mpaka tarehe 30/2/2024.
2. Kwamba, pande zote mbili za mkataba huu zimekubaliana kuwa kodi itakuwa Tshs. 600,000/= kwa mwezi.
3. Kwamba, kodi ya mwaka mmoja itakuwa fedha za Kitanzania Tshs. 7,200,000/=
4. Kwamba, mpangaji atapaswa kuwa analipa kodi kila baada ya miezi/mwezi 6.
5. Kwamba, kodi inayolipwa ni ya kipindi cha miezi sita (6) kuanzia tarehe 1 mwezi wa 2 mwaka 2023 hadi tarehe 30 mwezi wa 7 mwaka 2023.
6. Kwamba, kwa kusaini mkataba huu mwenye nyumba/chumba anakiri kupokea kodi ya miezi 6 kiasi cha Tshs. 3,600,000/=.
7. Kwamba, mpangaji atawajibika kulipa kodi zote na malipo yote ya serikali yanayotokana na malipo ya kodi hii nje ya kodi ya pango atakayokuwa akilipa.

8. Kwamba, mwenye nyumba/chumba atakuwa akitoa risiti kwa kila malipo atakayo pokea kutoka kwa mpangaji.
9. Kwamba, endapo muda wa mkataba utafikia ukomo na pande zote zikakubaliana kuongeza muda wa mkataba, masharti ya mkataba yanaweza kubadilishwa au yakabaki vile vile kutegemeana na pande zote zitakavyokubaliana.
10. Mpangaji atatumia eneo husika kwa matumizi ya **makazi/biashara**.
11. Mpangaji anapaswa kulipa ankara ya umeme, maji safi na maji taka kwa muda wote wa mkataba huu kulingana na matumizi yake.
12. Mpangaji atawajibika kutunza mazingira ya nyumba/chumba inayopangishwa/kinachopangishwa katika hali ya usafi na ubora kwa moda wote ambao atakuwa amepanga.
13. Kwamba, iwapo pataibuka mgogoro wowote baina ya pande mbili za mkataba huu basi pande zote zinakubaliana kutumia njia ya usuluhishi kama hatua ya awali ya utatuzi wa mgogoro na iwapo usuluhishi utashindikana basi kila upande utakuwa huru kuchukua hatua zingine stahiki za kisheria.
14. Kwamba, mkataba huu utalindwa kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

KWA KUSHUHUDIA YALIYOANDIKWA HUMU PANDE ZOTE MBILI WAMETIA SAINI ZAO KAMA IFUATAVYO KWA TAREHE MWEZI NA MWAKA KAMA ILIVYOONYESHWA HAPA CHINI.

IMETIWA SAINI na kutolewa hapa Dodoma)
na M/S THAKER SINGH ninayemfahamu/ambaye)
ametambulishwa kwangu na _____)
ninayemfahamu mbele yangu leo tarehe 01 mwezi)
02 mwaka 2023)

MUHURI
THAKER SINGH
P.O. Box 62
DODOMA

Saini: *Balvinder Singh Viridi*
Jina: BALVINDER SINGH VIRIDI
Anuani: P.O. Box 62,
DODOMA.
Cheo: DIRECTOR.

